# TATHMINI YA SHULE YA MSINGI
# ZOEZI YA NYUMBANI 2026
# GREDI YA 6 – KISWAHILI LUGHA
## Muda: Saa 1 Dakika 40

### TAARIFA ZA MWANAFUNZI

Jina: ______________________________ Shule: ______________________________

Nambari ya Tathmini: ______________________________ Tarehe: ______________________________

Nambari ya Shule: ______________________________ Sahihi: ______________________________

**MAELEKEZO KWA WANAFUNZI**

1. Andika jina lako, jina la shule yako na nambari yako ya mthani katika nafasi ulizoachiwa.
2. Andika tarehe,nambari ya shule yako kisa weka sahihi yako.
3. Soma kila swali kwa makini
4. Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote kwenye kijitabu hiki zimepigwa chapa.
5. Jibu maswali yote katika kijitabu hiki.

**JEDWALI LA ALAMA**

| SEHEMU | INSHA | LUGHA | KUSI/KUZU | ASILIMIA (%) | KUZ 1 | KUZ 2 | KUF 1 | KUF 2 | KUK 1 | KUK 2 | CHI 1 | CHI12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KIWANGO CHA ALAMA | ALAMA 20 | ALAMA 30 | ALAMA 30 | | 90-100 | 75-89 | 58-74 | 41-57 | 31-40 | 21-30 | 11-20 | 1-10 |
| POINTI | | | | | 8 POINTI | 7 POINTI | 6 POINTI | 5 POINTI | 4 POINTI | 3 POINTI | 2 POINTI | 1 POINTI |
| JUMLA YA ALAMA ZA MWANAFUNZI | | | | | | | | | | | | |

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu swali la 1 hadi la 5.**

*(Pendo yuko katika duka la Bwana Migwi)*

**Pendo:** Shikamoo Bwana Migwi!

**Bwana Migwi:** (Akimnyoshea mkono) Marahaba bimdogo. Je, jina lako ni lipi na ungependa nikusaidie vipi?

**Pendo:** Jina langu ni Pendo Kazuri. Mimi ni mwanafunzi wa Gredi ya sita katika shule ya Hekima. Nimekuja kujifunza kutoka kwako umuhimu wa kulipa ushuru.

**Bwana Migwi:** (Anawazia wateja wawili kisha anaendelea) Karibu Pendo. Ni muhimu sana kwa kila mfanyabiashara kulipa ushuru. Je, unaweza kunitajia baadhi ya mambo ambayo serikali huwafanyia wananchi?

**Pendo:** Kwa hakika, serikali ina majukumu mengi. Kwanza ni kuimarisha miundomsingi kama barabara, huduma za umeme, hospitali na maji safi. Halikadhalika, serikali hushirikiana na wananchi kudumisha usalama kwa kuwa kinga na kinga ndipo moto utakapo.

**Bwana Migwi:** Hakika naona u binti mwerevu sana. Sasa ningependa ujue kwamba serikali haitamtumia majukumu hayo yote iwapo tutadinda kulipa ushuru. Sasa umeona umuhimu wa kulipa ushuru?

**Pendo:** Ndio Bwana Migwi. Nimetambua kuwa huduma nyingi zitakosekana watu wasipolipa ushuru. Mimi binafsi ninatamani kuwa mfanyabiashara maarufu kama wewe nikiwa mkubwa.

**Bwana Migwi:** Nakutakia kila la heri Binti Pendo. Mola atayajibu maombi yako.

**Pendo:** Nashukuru sana kwa maelezo yako Bwana Migwi. Sasa naomba kuondoka. Kwaheri.

**Bwana Migwi:** Kwaheri ya kuonana. (Pendo anaondoka)

1. Mazungumzo haya yalifanyika wapi?

A. Shuleni B. Njiani C. Nyumbani D. Dukani

2. Chagua neno la adabu na heshima lililotumika katika mazungumzo haya.

A. Mwanafunzi B. Shikamoo C. Nimekuja D. Maarufu

3. Kulipa ushuru kuna umuhimu gani kulingana na kifungu?

A. Huiwezesha serikali kuwahudumia wananchi
B. Husaidia biashara kupata faida kubwa
C. Humwondolea mtu shida ya kutiwa mbaroni
D. Biashara hupata wateja wengi

4. Kifungu hiki kinatufunza nini?

A. Jinsi ya kuimarisha biashara
B. Manufaa ya elimu
C. Umuhimu wa kulipa ushuru
D. Matatizo ya wafanyabiashara

5. Neno 'wateja' limetumika katika kifungu. Kisawe cha neno hilo ni;

A. Wachuuzi
B. Watoa ushuru
C. Wanunuzi
D. Watu

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 6 hadi la 9.**

Siku moja, mfalme aliwaalika paka na panya katika ikulu washiriki karamu ya siku ya kuzaliwa kwa mwanawe. Halikadhalika walikuwepo wageni wengine kutoka sehemu mbalimbali. Sherehe ilinoga kwelikweli. Vyakula na vinywaji vilikuwako kochokochoko. Wageni walikula na kucheza kwa furaha.

Mfalme aliamua kuwatembeza wageni katika kasri. Aliwaonyesha mapambo ya dhahabu, maghala ya nafaka na mavazi ya kifahari. Kila mmoja aliambiwa achague zawadi iliyompendeza kwenye kasri ili apewe zawadi hiyo na mfalme. Kumbe wakati walipokuwa wakizunguka, panya aliiba pete ya dhahabu ambayo mfalme aliithamini sana. Alikuwa ameridhi pete hiyo kutoka kwa babu yake ambaye alikuwa mfalme wa kwanza.

Mfalme alipogundua kuwa pete yake imeibwa, alipandwa na mori. Alitishia kuwaangamiza wageni wote na kupanga iwapo pete yake isingepatikana. Acha wageni waingiwe na hofu! Ungezisikia nyoyo zao zilivyodunda hata ukiwa mbali.

Paka ambaye aliijua njama za panya, alimrukia na kumparuza kwa kucha zake. Panya alipiga ukelele mkali nayo pete ikaruka kutoka mdomoni mwake. Mfalme alimtazama panya kwa ukali. Huyoo! Panya alitimua mbio kujinusuru huku paka akimfuata mbio unyounyo kujaribu kumshika. Mfalme aliwaomba msamaha wageni wake kisha sherehe ikaendelea.

6. Sherehe ilihusu nini?

A. Siku ya kuzaliwa kwa mfalme
B. Siku ya kutoa zawadi
C. Siku ya kuzaliwa kwa mtoto wa mfalme
D. Kupata mfalme mwingine

7. Ni kweli kuwa mfalme huyo alikuwa;

A. karimu
B. mchoyo
C. mwivu
D. mwoga

8. Kwa nini mfalme alipandwa na mori?

A. Wageni waliharibu vitu
B. Pete yake ilipotea
C. Paka na panya walikimbizana
D. Alijua panya ameiba vitu

9. Kitendo cha panya cha kuiba kibaya kwa kuwa;

A. pete ile haikuwa muhimu
B. alifika bila kualikwa
C. alifanya paka ashukiwe
D. aliwatia wengine kwenye shida

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 10 hadi 12.**

Binadamu huweza kujibebea mambo mengi moyoni mwake. Baadhi ya mambo hayo huwa mazuri ilhali mengine huwa mabaya. Mambo mazuri ni kama furaha, upendo, amani, ukarimu na utu. Mtu akiwa na mambo hayo moyoni hupata marafiki wengi. Uso wake huonyesha tabasamu wakati wote.

Kwa upande mwingine, kuna watu ambao hubebesha mioyo yao mizigo mizito ya maovu. Mifano ya maovu hayo ni chuki, ukatili, matusi, kisasi na ubinafsi. Mambo haya huwa kama moto ambao huchoma moyo wa mtu huyo na kumletea maradhi. Watu wanaobeba maovu kama haya wanaweza kujipata wakiugua maradhi ya moyo na shinikizo la damu.

10. Binadamu hujibeba nini moyoni?

A. Mambo mazuri pekee
B. Mambo mabaya pekee
C. Mema na maovu
D. Maradhi mbalimbali

11. Kifungu hiki kimefanisha mambo maovu na nini?

A. Moto unaochoma
B. Maradhi ya moyo
C. Shinikizo la damu
D. Kisasi na ubinafsi

12. Chagua jibu lisilo sahihi kulingana na kifungu.

A. Watu wanaoibeba mazuri moyoni hupendwa na wengi
B. Watu wanaopenda maovu huweza kukosa marafiki
C. Kukosa furaha kunaweza kusababisha shida za kiafya
D. Watu wote wanaopata maradhi huwa na mabaya moyoni

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 13 hadi la 15.**

Faraja alisikitishwa sana na baadhi ya vijana wa kijiji chao. Vijana wale walitumia sigara, pombe, miraa na mihadarati nyingine. Baadhi yao walijipata wakijibizana na wazazi wao bila aibu. Badala ya kuwasaidia wazazi katika kazi, wengine wao walizurura mjini kama mbwakoko wakitafuta dawa za kulevya. Walianza kuwa na mkono mrefu ili wapate pesa za kugharamia ulevi wao.

Kibe aliwaza kwa muda. Mwishowe aliamua kuwashauri vijana wale. Aliwatembelea mmoja mmoja nyumbani kwao. Awali, vijana wale hawakutaka kumsikiliza. Lakini alijua kuwa mvumilivu hula mbivu. Juhudi zake zilianza kuzaa matunda. Vijana wale walianza kubadilika polepole. Waliomba msamaha kwa wazazi wao. Badala ya kurandaranda, walianzisha vilabu vya michezo. Waliacha wizi wakaanza kuwasaidia wazazi wao.

13. Ni jambo lipi lililomsikitisha Kibe?

A. Vijana wenzake walipotoka
B. Ndugu zake walijibizana na wazazi
C. Vijana wote walitumia mihadarati
D. Hakuwa na marafiki kijijini

14. Ipi haikuwa tabia ya vijana wanaozungumziwa?

A. Kulewa
B. Kuiba
C. Kuwasaidia wazazi
D. Kuzurura ovyo

15. Kifungu hiki kinatuhimiza tufanye nini?

A. Tuwaepuke watu wabaya
B. Tuwashauri watu wabaya wabadilike
C. Tukae nyumbani bila kufanya lolote
D. Tujibizane na wazazi

**Kuanzia nambari 16 hadi 20, jaza vihasho kwa jibu lililo sahihi zaidi.**

Wakulima wale ***16*** kutayarisha ***17***. Ushirikiano ***18*** ulidhihirisha ukweli wa methali isemayo ***19***. Msimu wa ***20*** ulipofika, mvua ilinyesha kwa wingi mimea yao ikanawiri.

| **No.** | **A** | **B** | **C** | **D** |
|---|---|---|---|---|
| 16 | mlishirikiana | alishirikiana | tulishirikiana | walishirikiana |
| 17 | shamba zao | mashamba yao | mashamba zao | shamba vyao |
| 18 | hayo | hiyo | huo | hizo |
| 19 | umoja ni nguvu | bidii hulipa | baada ya dhiki faraja | maji yakijaa hupwapwa |
| 20 | kiangazi | vuli | kipupwe | masika |

21. Chagua nomino za ngeli ya U - U.

A. Ugonjwa, upishi
B. Wali, uhuru
C. Upishi, ulezi
D. Waya, wimbo

22. Andika wingi wa sentensi ifuatayo; Mvua ilinyesha nikaingia nyumbani.

A. Mvua zilinyesha nikaingia nyumbani
B. Mvua ilinyesha tukaingia manyumbani
C. Mvua zilinyesha tukaingia manyumbani
D. Mvua ilinyesha tukaingia nyumbani

23. Mkufu huvaliwa wapi?

A. Shingoni
B. Nyweleni
C. Mkononi
D. Mguuni

24. Kanusha; Mpunga uliunwa jana.

A. Mpunga haunwi jana
B. Mpunga hautavunwa jana
C. Mpunga haukuvunwa jana
D. Mpunga haujavunwa jana

25. Msemo upi una maana ya 'kukubaliana katika jambo''?

A. Sema kwa sauti moja
B. Changa bia
C. Kunja jamvi
D. Chapa kazi

26. Ni sentensi ipi iliyo sahihi?

A. Hapa kuna miti mingi
B. Humu pana mti mingi
C. Huku pana miti mingi
D. Hapa pana miti mingi

27. Kitenzi 'funga' katika kauli ya 'kutendesha' kitakuwa;

A. fungua
B. funghisha
C. fungia
D. fungulia

28. Andika kinyume cha neno lililopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo; Mpishi alikata mboga kwa kisu kikali.

A. Kibaya
B. Kizuri
C. Butu
D. Kizee

29. Badilisha sentensi ifuatayo katika hali ya udogo. Mbwa wenu ametibiwa.

A. Jibwa lenu limetibiwa
B. Kijibwa chenu kimetibiwa
C. Jibwa wenu ametibiwa
D. Kijibwa wenu kimetibiwa

30. Neno lipi ni kivumishi katika sentensi hii?

A. Shamba
B. Lina
C. Miti
D. Mirefu

**MAJIBU**

1. D
2. B
3. A
4. C
5. C
6. C
7. A
8. B
9. D
10. C
11. A
12. D
13. A
14. C
15. B
16. D
17. B
18. C
19. A
20. D
21. B
22. D
23. A
24. C
25. A
26. D
27. B
28. C
29. B
30. D